KENYA JUNIOR SCHOOL EDUCATION ASSESSMENT

GRADE 8 – 2026

KISWAHILI (INSHA NA UCHANGANUZI WA FASIHI)

KARATASI YA 2

MUDA: Saa 1 dakika 45

Jina la Mwanafunzi	_____	Nambari ya Mwanafunzi	_____
Jina la Shule	_____	Nambari ya Shule	_____
Sahihi ya Mwanafunzi	_____	Tarehe	_____

MAAGIZO KWA WANAFUNZI

1. Andika jina lako na nambari yako ya mtihani kwenye nafasi zilizoachwa hapa juu.
2. Andika jina na nambari ya shule yako kwenye nafasi zilizoachwa hapa juu.
3. Tia sahihi kwenye nafasi iliyoachwa hapo juu.
4. Andika tarehe ya mtihani ipasavyo.
5. Karatasi hii ina sehemu mbili; A na B.
6. Jibu maswali yote.
7. Andika majibu yote kwenye nafasi ulizoachwa katika kijitabu hiki.
8. Majibu yote ni lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

KWA MATUMIZI YA MTATHMINI PEKEE

SEHEMU	A	B	B	B	B
ZOEZI	Zoezi I	Zoezi II	Zoezi III	Zoezi IV	Zoezi V
Alama ya upeo	15	10	10	10	5

Jumla: 50 ALAMA

SEHEMU A: INSHA (Alama 15)

ZOEZI I: INSHA

Maagizo:

Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.

Andika insha yenye maneno kati ya 300–350.

Andika insha itakayomalizika kwa:

"…nilitambua kwamba uaminifu hujenga heshima katika jamii."

SEHEMU B: FASIHI (Alama 35)

ZOEZI II: FASIHI SIMULIZI (Alama 10)

Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Jamii ya Mogo inaamini kuwa Mungu wao ‘Monene’ alimuumba mwanamume aliyeitwa Sacha na mwanamke aliyeitwa Kungu. Mke na mume waliishi kwa raha na furaha. Walijaliwa wana wa kiume watano. Sacha alikuwa mvuvi maarufu. Alitegemea uvuvi na kilimo kulisha familia yake. Wavulana hao walipoendelea kukua ndivyo woga ulivyowaingia. Hawakujua kizazi chao kingeendelea vipi na hapakuwa na wasichana wa kuoa. Sacha alianza kumwomba ‘Monene’ awaumbie wavulana wake wasichana wa kuoa.

Kama ilivyo ada, mwana wa mhunzi asiposana, huvuvia. Wavulana wale waliipenda kazi ya uvuvi. Walitii maagizo ya wazazi wao. Walikuwa waogeleaji maarufu na hivyo hawakuogopa maji. Walikuwa na bidii ya mchwa. Bahari ile ilikuwa na samaki wengi. Kila siku walirudi nyumbani na mtungo wa samaki. Baba yao alifurahi sana kwa sababu alipunguziwa kazi ya kuvua. Alipata nafasi kupumzika na kusaidiana na mkewe kufanya shughuli za kilimo.

Siku moja ilikuwa ajabu kwa vijana hao. Ilikuwa ni usiku wa manane. Hawakupata hata samaki mmoja. Samaki walihepa nyavu zao na kuwapeleka hadi katikati ya bahari. Hawakuelewa sababu ya samaki kuwa wajanja kiasi hicho. Hawakujua wangewaambia wazazi wao nini. Walijipa moyo na kuendelea kujaribu.

Walijikuta katikati ya bahari. Ghafla bin vuu, walimwona msichana mrembo kama malaika akiogelea. Msichana mwingine aliibuka. Jambo la ajabu zaidi ni kuwa wasichana wale walikuwa wameagizwa na Monene kwenda kuolewa nao.

Wasichana waliingia katika mashua ambazo zilikuwa zikiwasubiri samaki, walishangaa kuwaona vijana wale. Walisimulia kilichotokea. Walifurahi upeo wa furaha. Waliandaa sherehe kubwa kuwakaribisha wakwe zao. Kila mmoja alijenga nyumba yake na kuanzisha familia yake.

9. a) Hadithi hii inaonyesha imani za jamii kuhusu asili ya binadamu. Taja jambo moja linalodhihirisha imani hiyo. (alama 2)

_____
_____

_____
_____

10. b) Eleza umuhimu wa uvuvi katika maisha ya familia ya Sacha. (alama 2)

_____
_____

_____
_____

11. c) Taja sifa mbili za vijana wa Sacha zinazojitokeza kutokana na matendo yao. (alama 2)

_____
_____

_____
_____

12. d) Eleza mabadiliko mawili yaliyotokea baada ya vijana hao kukutana na wasichana. (alama 2)

_____
_____

_____
_____

13. e) Tambua mbinu mbili za lugha zilizotumiwa katika hadithi na utoe mifano kutoka katika hadithi. (alama 2)

_____
_____

_____
_____

ZOEZI III: NOVELA (Alama 10)

Soma dondoo lifuatalo ya novela kisha ujibu maswali yanayofuata.

Daktari alimlaza Chale kwenye kitanda. Alichukua stethoskopu yake kisha akampima Chale. Alikiweka kipimamwili chenyewe kando na kumbinyabinya mguu. Chale aliuvuta mguu wake kiasi na daktari akaelewa kwamba alikuwa akihisi uchungu. Baada ya kuridhika na uchunguzi, daktari alimtoa Chale kwenye kitanda na kumketisha kwenye kiti kilichokuwa karibu na chake.

“Nimemchunguza kijana huyu. Mguu huu hauelekei kuwa umeteguka au kuumia kwa namna nyingine yoyote. Umevimba tu. Tutahitaji kumfanyia uchunguzi wa kina ili kubaini kiini cha uvimbe huo. Inaonekana kwamba tatizo hasa liko kwenye kifundo na sehemu yote inayounganisha wayo na muundi. Kwa sasa nitawapa dawa ya kupunguza maumivu na joto. Nitawapa pia barua ya kumpeleka kwenye hospitali kuu ya kaunti ili afanyiwe uchunguzi wa kina zaidi na kupewa matibabu yafaayo. Huenda akahitaji kulazwa hospitalini ili kurahisisha kupata vipimo na kushughulikiwa kwa dharura,” daktari aliwaeleza wazazi wa Chale.

Wazo la kulazwa hospitalini lilimshtua Chale. Hata hivyo, alijambia kwamba heri kulazwa hospitalini kuliko kuzikwa kwa ndoto zake za utangazaji. Sitosheke, uchungu ulikuwa unamtatiza. Macho yao yalihakikisha kwamba huo ndio uliokuwa uamuzi uliofaa zaidi wakati huo. Walimwinua kutoka kitini, wakamuaga daktari na kuelekea kwenye kidirisha ambako kulikuwa kunatolewa dawa.

Akiwa nyumbani, Chale alitamani jua lichomoze kabla ya wakati wake wa kawaida. Dawa alizopewa za kupunguza maumivu zilikuwa jino la pembe. Zilimtuliza kwa muda tu halafu mguu ukaanza kupwita zaidi. Hata jimbi wa kwanza alipotangaza mapambazuko ya siku mpya, Chale alimshukuru Maulana kwa kuona kwamba msaada wake ulikuwa karibu.

a) Eleza tatizo kuu la Chale linalojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)

_____
_____

_____
_____

b) Fafanua dhamira moja inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)

_____
_____

_____
_____

c) Tambua tamathali tatu za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili. (alama 3)

_____
_____

_____
_____

d) Eleza mandhari mbili zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)

_____
_____

_____
_____

e) Taja sifa moja ya Chale inayodhihirika katika dondoo hili. (alama 1)

_____
_____

_____
_____

ZOEZI IV: TAMTHILIA (Alama 10)

Soma sehemu hii ya tamthilia kisha ujibu maswali yanayofuata.

Zake: (Anasema kwa kĕshtosita.) Nadhani walisigizia tu ugonjwa huo. Ninahisi kuwa amenifukiza kwa sababu wanapika chapati na kuku.

Neema: Chapati tu? Chakula ambacho watakula na kupeleka chooni? (Anamuliza.) Sikiliza baba, wewe ukiwa ugali kwa kisamvu na wao wale hizo chapati kwa kuku, mtu atajua mmekula vyakula tofauti kwa kuratwazama?

Zake: (Anatikisa kichwa kutoridhika.) Hahaha!

Neema: Kule msalani, choo yao takaliwa na nyama ya kuku na yako iwe na majani ya kisamvu?

Zake: Hataa! Nyote mtakuwa sawa tu!

Neema: Basi huo ni moja kati ya miujiza ya Mungu. Hatufai kuhuzunishwa na hali za watu. Leo huyo mwenye kutucheka atakunywa chai ya maziwa, soda au sharubati. Sisi hapa tunakunywa uji na maji ya mtoni. Mbali na hayo, sote tunaenda shule moja na kufonzwa na walimu wale wale. Sote tunapumua hewa sawa. Je, mkienda kubagua, hao kina Kibano watatoa mkojo wa juisi nawe wako ukapiga hudhurungi wa maji ya mto?

Tito: (Akimpigia Zake.) Hilo haliwezekani.

Neema: Hapo sasa! Ndiyo nasi tufahamu kuwa mbele yake Mungu, sote tupo sawa. (Anamkumbatia Neema.) Asante dada Neema. Huwa unatutia moyo hata wakati tumaini halipo.

Neema: Ni wajibu wangu tu. Ukubwa ni jaa.

Tito: Kweli dada. Katika ulimwengu huu wa leo, walimwengu na malimwengu yao ni balaa.

Neema: Kila kitu ni balaa nakwambia. Walimwengu balaa. Ulimwengu pia ni balaa hata nikautungia wimbo!

Tito: Nao wimbo wenyewe ukaibuka wa kwanza katika mashindano ya kieneo, sawa na shairi langu.

Zake: (Kwa sauti ya kusinzia.) Nakumbuka mlileta soda na mkate siku hiyo ya mashindano.

Neema: (Anaonyesha kushtuka kwa kukumbuka jambo. Anashusha pumzi kwa nguvu na kumgeukia Tito.) Jamani, ni siku chache zimesalia kabla ya tamasha ya kitaifa ya nyimbo na mashairi. Tutakuwa tunawasilisha na ninahisi hatujafanya maandalizi ya kutosha.

Tito: Napendekeza tumalize kazi za nyumbani kisha utuwasilishie tena wimbo wenyewe. Mimi pia nitawasilisha shairi langu kuhusu mtoto wa kiume ili mnitoe maoni.

Neema: Wazo zuri. Sisi kwetu ni wana wa mhunzi. Tusiposana tutavuvia. Natumai baba atakuwa amefika ili tupe maelekezo ya jinsi alivyofanya wakati wa mashindano ya kieneo.

a) Eleza masuala mawili yanayojitokeza katika sehemu hii ya tamthilia. (alama 4)

_____
_____

_____
_____

_____
_____

b) Tambua mbinu tatu za lugha zilizotumiwa katika sehemu hii na utoe mifano. (alama 3)

_____
_____

_____
_____

_____
_____

c) Eleza umuhimu wa ploti katika kujenga ujumbe wa sehemu hii ya tamthilia. (alama 3)

_____
_____

_____
_____

_____
_____

ZOEZI V: USHAIRI (Alama 5)

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Tulia mfano wa maji, kwenye mtungi hakika,
Wewe ni mnunuaji, muuza ni mwenye duka,
Usionyeshe ujuaji, uwache kulalamika,
Mchambua nazi sana, huzichagua koroma.

Bidhaa unapohitaji, ni vyema kuwajibika,
Pamoja na muuzaji, teua unachotaka,
Kwa heshima umhoji, bila tatizo kuzuka,
Mchambua nazi sana, huzichagua koroma.

Piga bei kwa mwenyeji, na uwe nayo mipaka,
Mwenyewe ni muuzaji, na biashara ‘meweka,
Faida nayo haiji, bila huo ushirika,
Mchambua nazi sana, huzichagua koroma.

Uchunguze upambaji, wa kitu unachotaka,
Ni soda au kabeji, epuka kushikashika,
Kweli utavikwa taji, kama utawajibika,
Mchambua nazi sana, huzichagua koroma.

Ya ziada siyataji, tamatini nimefika,
Wala sinacho kipaji, nasema yakusikika,
Ushauri kihitaji, mkono nitakushika,
Mchambua nazi sana, huzichagua koroma.

a) Ni tabia zipi mbili za mnunuzi anayependekezwa na mshairi? (alama 2)

_____
_____

_____
_____

b) Andika kibwagizo cha shairi hili. (alama 1)

_____
_____

_____
_____

c) Kwa kuzingatia idadi ya mishororo katika kila ubeti, shairi hili ni la aina gani? Eleza. (alama 2)

_____
_____

MWISHO WA KARATASI